OFISI YA RAIS TUME YA MIPANGO

MWENENDO WA UCHUMI WA TANZANIA NA MWELEKEO WA BAADAYE WA UTEKELEZAJI WA DIRA YA TAIFA YA MAENDELEO 2025

MKUTANO WA MABALOZI WA TANZANIA
HOTELI YA RAMADA – DAR ES SALAAM
25 -26 MEI, 2015

MPANGILIO WA MADA

- Mwenendo wa Uchumi wa Tanzania
  - Sura ya Uchumi
  - Mwenendo wa Viashiria Vikuu vya Kiuchumi
  - Majumuisho
- Mwelekeo wa Baadaye wa Utekelezaji wa Dira 2025
  - Malengo ya Dira 2025 na Mpango Elekezi
  - Mwelekeo wa Mpango wa Pili wa Miaka Mitano (2016/17 – 2020/21)
- Nafasi ya Mabalozi Katika Utekelezaji wa Dira 2025
  - Diplomasia ya Kiuchumi
  - Mwongozo wa Jumla
- Hitimisho

1. Mwenendo wa Uchumi wa Tanzania

1.1 Sura ya Uchumi 2005-2014

- **Pato la Taifa = $43,702.8m (2013), sawa na kipato cha wastani wa $948 kwa kila mtu (Tanzania Bara), ikilinganishwa na kipato cha $709 (2010)**

- **Tanzania inakaribia kuingia kwenye kundi la chini la nchi zenye hadhi ya kipato cha kati ($1,036 - 4,085) – *Low Middle Income Countries*!!**

- **Angalizo: Tusibweteke! Kiwango cha umasikini nchini bado ni kikubwa japo kimepungua (mijini & vijijini) kutokana na kasi kubwa ya ukuaji wa uchumi (wastani wa 6.5% kwa mwaka) kwa kipindi cha takriban miongo miwili. Umaskini wa mahitaji ya msingi (*BNP*) umepungua kutoka 34% (2007) hadi 28% (2012). Hata hivyo, WB inakadiria kuwa 90% ya Watanzania wanapata kipato pungufu ya $3 kwa siku. Vile vile, changamoto za kilimo duni, miundombinu hafifu, mahitaji makubwa ya huduma bora za maji, afya, elimu n.k bado ni kubwa.**

- **Hivyo, jitihada kubwa zaidi zinahitajika kufikia lengo lililowekwa kwenye Dira ya Taifa ya Maendeleo la kufikia kipato cha $3,000 ifikapo 2025.**

Umasikini Umepungua (mijini & vijijini)



	2007	2011/12
Umasikini (%)	**34.4**	**28.2**
Umasikini Uliokithiri (%)	**11.7**	**9.7**



	2007	2011/12
Umasikini vijijini (%)	**39.4**	**33.4**
Umasikini Dsm (%)	**14.1**	**4**
Umasikini miji mingine (%)	**22.7**	**21.5**

Sura ya Uchumi 2005 na 2014





Sura ya Uchumi 2005-2014

•**Mchango wa sekta za huduma (biashara ya jumla & rejareja, usafirishaji & uhifadhi, hoteli & migahawa, habari & mawasiliano, shughuli za fedha & bima, mali isiyohamishika, utawala & ulinzi, sanaa & burudani, upatikanaji wa maji & umeme, n.k. ndiyo inayochangia sehemu kubwa ya pato la Taifa – takriban 41.3% ya pato la Taifa (2014) ikilinganishwa na 47.8% (2005).**

•**Mchango wa sekta ya kilimo katika Pato la Taifa kwa ujumla umebaki palepale katika kipindi cha muongo mmoja uliopita yaani 28.9% (2014) ikilinganishwa na 28.6% (2005). Mchango wa sekta ndogo ya mazao ndiyo sehemu kubwa takriban 16.2%, ikifuatiwa na mifugo (7.4%), misitu (3.1%) na uvuvi (2.2%).**

- **Mchango wa sekta ya viwanda (manufacturing) katika Pato la Taifa umepungua** kutoka 7.3% (2005) hadi 5.6% (2014) kutokana na kuongezeka kwa michango ya baadhi ya sekta (e.g. ujenzi, misitu) na pia sekta mpya kiungizwa katika takwimu za pato la Taifa (e.g. sanaa na burudani).

- **Mchango wa sekta ya ujenzi katika pato la Taifa umeongezeka** kutoka 7% (2005) hadi 12.5% (2014)

1.2 Mwenendo wa Viashiria vya Kiuchumi

Ukuaji wa Pato la Taifa 2006-2014

Pato la Taifa lilikua kwa wastani wa 6.4% kwa mwaka (2006-2014) ikiwa ni chini ya lengo la 8% kwa mwaka lililowekwa katika Dira 2025.

Hata hivyo, ukuaji huo umeiwezesha Tanzania kuwa miongoni mwa nchi 20 duniani ambazo uchumi wake unakuwa kwa kasi kubwa na kuzidi wastani wa ukuaji wa uchumi kwa nchi za Afrika kusini mwa jangwa la Sahara.

Ukuaji wa Pato la Taifa



Ukuaji huo kwa kiasi kikubwa kumechangiwa na:

- **Kuendeleza utulivu wa uchumi-jumla ikiwa pamoja na kudhibiti mfumuko wa bei, nakisi ya bajeti na usimamizi imara wa sekta ya fedha;**

- **Uboreshaji wa mifumo ya kitaasisi, sheria na usimamizi (institutional, legal & regulatory frameworks);**

- **Jitihada kubwa kujenga & kukarabati miundombinu, n.k); na**

- **Kuongezeka kwa uwekezaji hususan katika sekta za madini, gesi asili, uzalishaji wa bidhaa za viwandani, ujenzi, mawasiliano, uchukuzi, huduma za fedha, utalii na mali isiyohamishika (*real estate*).**

Sekta za huduma, ujenzi & viwanda zinaongoza Katika Ukuaji (%)

	2006	2007	2008	2009	2010	2011	2012	2013	2014	Wastani
Manufacturing	8.4	11.5	11.4	4.7	8.9	6.9	4.1	6.5	6.8	7.7
Construction	19.2	13.1	9.7	-3.8	10.3	22.9	3.2	14.6	14.1	11.5
Wholesale & retail trade	9.4	12.9	6.5	2.7	10	11.3	3.8	4.5	10	7.9
Transport & storage	9.1	2	1.8	6.9	10.7	4.4	4.2	12.2	12.5	7.1
Financial & insurance activities	19.1	21.7	18.8	18.4	12.6	14.8	5.1	6.2	10.8	14.2
Information & communication	4.5	17.7	11.9	26.6	24.4	8.6	22.2	13.3	8	15.2

Ukuaji Katika Baadhi ya Sekta (%)

	2006	2007	2008	2009	2010	2011	2012	2013	2014	Wastani
Agriculture	2.4	2.4	7.5	5.1	2.7	5.5	3.2	3.2	3.4	3.9
Mining & quarrying	-13.7	9.2	-9.8	18.7	7.3	6.3	6.7	3.9	9.4	4.2
Electricity supply	-8.7	18.7	8.1	4.3	13.4	-4.3	3.3	13	9.3	6.3
Arts, intertainment & recreation	5.3	7.5	6.4	3	7.3	7.7	11	5.7	5.7	6.6

Mfumuko wa Bei

Mfumuko wa bei umendelea kupungua kutoka wastani wa 12.7% (2011) na 16.0% (2012) hadi 7.9% (2013) na 6.1% (2014);

Bei za vyakula na nishati zimeendelea kuwa sababu kuu za mfumuko wa bei nchini;

Kushuka kwa bei za mafuta katika soko la dunia na kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao ya chakula nchini vimepunguza mfumuko wa bei 2013 na 2014. Mfumuko wa bei Desemba 2014 ulifikia 4.8%



Mauzo Nje & Akiba ya Fedha za Kigeni

- **Thamani ya mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi zimeongezeka kutoka $3,805m (2010) hadi $8,812.5m (2014)**

- **Sehemu kubwa ya mapato ya fedha za kigeni hivi sasa (2014) yanatokana na mauzo ya huduma hususan utalii ($1,950.1m) na biashara inayopita kwenda nchi jirani (transit trade), bidhaa za viwandani $1,434.3m na dhahabu ($1,282.1m). Mauzo ya mazao ghafi (pamba, kahawa, tumbaku, chai, katani, korosho) ambayo awali yalikuwa yanachangia 25% ya mapato ya fedha za kigeni hivi sasa yanachangia 10% tu.**

Bidhaa na Huduma Zilizoagizwa Kutoka Nje

Thamani ya bidhaa na huduma zilizoagizwa nje ya nchi (bidhaa za walaji, mashine, vyombo vya usafiri, malighafi za viwandani na mafuta) zimekuwa zikiongezeka kutoka $6,596m (2010) hadi $13,623.2 m (2014)

Akiba ya Fedha za Kigeni: Akiba ya fedha za kigeni imeongezeka kutoka $3,483m (2010) hadi = $4,388.6m (2014) ambayo inatosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma nje kwa miezi 4.1

Thamani ya Shilingi ya Tanzania: Kiwango cha kubadilisha $1 ya kimarekani kwa shilingi ya Tanzania katika soko la fedha za kigeni kimeendelea kuongezeka kutoka wastani wa shilingi 1,432.3 (2010) hadi shilingi 1,571.7 (2012) na shilingi 1,597.6 (2013). Thamani ya shilingi imezidi kushuka siku za karibuni. Kufikia tarehe 21 Mei 2015 $1 ilinunuliwa kwa shilingi 1,963.8. Changamoto kubwa hapa ni kupanua wigo wa mauzo ya bidhaa na huduma za Tanzania nje ya nchi ili kuhimili mahitaji katika soko la fedha za kigeni na kudhibiti ununuzi wa dola kwa kuotea (*speculation*)

Mapato ya ndani: Mapato ya ndani yameongezeka kutoka 11.5% ya pato la Taifa (2010) hadi 12.7% (2012) na 12.9% (2013). Takriban 91.5% ya mapato ya ndani yanatokana na kodi.

Matumizi ya Serikali: Matumizi ya Serikali 2010 yalifikia 20.1% ya pato la Taifa na 20.6 % (2013). Matumizi ya maendeleo ni takriban 6.2% ya pato la Taifa ikilinganishwa na matumizi ya kawaida ambayo ni 14.4% ya pato la Taifa. Uwiano wa bajeti ya maendeleo na bajeti yote unafanana na nchi nyingi kusini mwa jangwa la Sahara (Tanzania 31%, Kenya 30%, Ghana 31.4, Malaysia 19%, Thailand 17.5). Changamoto ni upatikanaji fedha kwa wakati na kuhakikisha kinachotekelezwa kinawiana na thamani ya fedha zilizotumika.

Deni la Nje: Limeongezeka kutoka $8bn (2010) hadi kufikia $10 (2012) na $19.48bn (Machi 2015). Sababu kubwa za ongezeko hili ni riba na madeni mapya yaliyokopwa hususan kugharamia ujenzi wa miundombinu ya usafirishaji na nishati.

1.3 Majumuisho Kuhusu Mwenendo wa Uchumi

- **Mwenendo wa uchumi wa Tanzania 2005 – 2014 unaonesha kuwa utekelezaji wa programu na mikakati mbalimbali hususan usimamizi wa uchumi-jumla, ujenzi & ukarabati wa miundombinu ya usafirishaji, umeme, elimu, afya na maji n.k umejenga misingi imara ya kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025.**

- **Hata hivyo, pamekuwepo changamoto mbalimbali katika hatua ya utekelezaji kama vile vyanzo hafifu vya mapato (ndani na nje), kushindwa kutumia kikamilifu fursa za PPP, malimbikizo ya madai ya wakandarasi, na misukosuko katika uchumi wa dunia.**

2. Mwelekeo wa Baadaye wa Utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025

2. 1 Malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025

A: Maisha bora na mazuri

- **Lengo 1**: Kujitosheleza kwa chakula;
- **Lengo 2**: Elimu ya msingi kwa wote, kufuta ujinga & kufikia kiwango kinachoridhisha cha elimu ya kati na juu;
- **Lengo 3**: Usawa wa kijinsia na kuwapa fursa wanawake kushiriki katika masuala yote ya kijamii, kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni;
- **Lengo 4**: Upatikanaji wa huduma za msingi kwa watu wote;
- **Lengo 5**: Upatikanaji wa huduma bora za uzazi kwa watu wote wenye umri unaostahili;
- **Lengo 6**: Kupunguza vifo vya watoto wachanga na vifo vya uzazi kwa robo tatu ya viwango vya sasa;
- **Lengo 7**: Upatikanaji wa maji salama kwa watu wote;
- **Lengo 8**: Kuongeza wastani wa umri wa kuishi kulingana na kiwango kilichofikiwa na nchi zenye mapato ya kati;
- **Goal 9**: Kuondoa kabisa umasikini uliokithiri.

B: Uongozi bora & utawala wa kisheria

- **Lengo 1**: Maadili mema na kuthamini utamaduni;
- **Lengo 2**: Uadilifu na kuheshimu utawala wa sheria;
- **Lengo 3**: Kutokuwepo rushwa na maovu mengine;
- **Lengo 4**: Jamii iliyoelimika na inayojiamini, inayojifunza kutokana na uzoefu wake na wa wengine na wenye kumiliki na kubaini agenda ya maendeleo yake.

C: Uchumi imara na wenye uwezo wa ushindani

- **Lengo 1**: Kuwa na vianzio mbalimbali vya uzalishaji na uchumi ambao una maendeleo ya viwanda yaliyo karibu sawa na nchi zenye mapato ya kati;
- **Lengo 2**: Utangamano wa uchumi unaojidhihirisha kwa kuwepo kwa kasi ndogo ya mfumuko wa bei na uwiano madhubuti wa uchumi kwa ujumla;
- **Lengo 3**: Ukuaji wa uchumi wa asilimia 8 au zaidi kwa mwaka;
- **Lengo 4**: Kuwepo kwa miundombinu ya kutosha kuweza kukidhi mahitaji ya malengo ya Dira katika sekta zote;
- **Lengo 5**: Mshiriki na mshindani shupavu katika masoko ya nchi jirani na ya dunia kwa ujumla. Inatarajiwa pia kwamba ukuaji haraka wa uchumi utakwenda sawia na urekebishaji wa uharibifu wa mazingira na rasilimali.

(2010)	FYDP I (2011/12 – 2015/16) Kufungulia fursa za ukuaji wa uchumi	FYDP II (2016/17 – 2020/21) Kujenga Misingi ya uchumi wa viwanda	FYDP III (2021/22 -2025/26) Kujenga Uchumi shindani unaoongozwa na mauzo nje
Uchumi unaotegemea kilimo	Kuondoa vikwazo vya ukuaji wa uchumi (umeme, bandari, barabara vijijini, reli, sayansi,teknolojia & ubunifu, TEHAMA)	Kuongeza kasi ya ukuaji wa sekta ya viwanda	Kuboresha ushindani wa kiuchumi kikanda & kimataifa
Miundombinu hafifu (umeme, bandari, barabara vijijini, reli, TEHAMA)	Kuongeza tija katika kilimo na ushindani ili kuwa ghala la chakula katika ukanda huu wa Afrika	Kujenga viwanda vya kuchakata & kuongeza thamani ya mazao, mifugo, uvuvi, misitu na kuchenjua madini	Kuwezesha uchumi kukua ukiongozwa na mauzo nje
Changamoto za utawala bora	Kuandaa Taifa kuvuna rasilimali zake (gesi, chuma, makaa ya mawe, magadi soda & madini) kwa ufanisi	Kujenga viwanda vinavyotumia teknolojia ya kati	Kuongeza mchango wa Tanzania katika biashara ya kimataifa
Kiwango kikubwa cha ukosefu wa ajira	Kujenga ujuzi wa rasilimaliwatu	Kujielekeza kujenga viwanda mama - chuma, kemikali na vile vinavyotokana au kuchochewa na gesi asili	Kuibadilisha kabisa Tanzania kuwa kitovu cha uzalishaji viwandani Afrika Mashariki
Tija ndogo katika sekta zote; Sekta changa ya viwanda; Rasilimaliwatu isiyo na ujuzi; Muunganiko hafifu kati ya sekta	Kuweka mazingira mazuri ya biashara & uwekezaji	Kuongeza thamani ya madini yote yanayozalishwa nchini	Kilimo chenye tija kubwa

2.2 Mwelekeo wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17 – 2020/21)

2.2.1 Fursa Zitakazo Zingatiwa Katika Mpango

- Rasilimali nyingi- Ardhi ya Kilimo, Maji ya Umwagiliaji, Misitu, Wanyama Pori, Madini.
- Jiografia- Lango Kuu la Biashara na Huduma kwa nchi za Maziwa Makuu
- Nguvu kazi kubwa (hasa vijana) yenye gharama nafuu.
- Soko kubwa la Kikanda – Afrika Mashariki, SADC
- Ukuaji wa miji – ongezeko la wananchi wenye kipato cha kati mijini na mahitaji zaidi ya bidhaa na huduma na pia mazingira ya kuanzisha na kukuza viangulia vya viwanda na SMEs
- Uhusiano mzuri na nchi mbalimbali hasa China, India, Brazil, SA na nchi zinazoibukia (Malaysia, Indonesia, Vietnam, n.k.) zenye nguvu kubwa za kiuchumi
- Amani na utulivu nchini

2.2.2 Vihatarishi

- Athari za mabadiliko ya tabianchi (ukame/ uhaba wa maji, mafuriko);
- Uchafuzi wa mazingira;
- Kuongezeka kwa matukio ya Ugaidi na vita;
- Kasi kubwa ya ongezeko la Idadi ya Watu Mijini bila Viwanda/ Ukosefu wa ajira;
- Kuongezeka kwa tofauti za kipato

2.3 Mkakati wa Kujenga Misingi ya Uchumi wa Viwanda

2.3.1 Aina ya Viwanda

- Kuelekeza nguvu kujenga Viwanda vinavyotumia malighafi za hapa nchini na vinavyotumia nguvu-kazi zaidi (*Food Manufacturing*, kuongeza thamani ya mazao ya kilimo, viwanda vya nyama na ngozi, kusindika samaki, mazao ya misitu);

- Kuongeza kasi ya kujenga *SEZs/EPZ, Industrial & ICT parks,* n.k. na kuvutia uwekezaji kutoka nje;

- Kuvutia Viwanda vinavyotumia nguvu-kazi kutoka Asia (*sun set industries*) na kujenga maghala makubwa ya biashara;

- Kujenga Viwanda vidogo na vya kati kwa ajili ya wakazi wa mijini na vijijini;

- Kujenga Viwanda vya kuzalisha bidhaa zenye soko kubwa katika ukanda huu wa Afrika;

- Kujenga Viwanda-mama vinavyotumia rasilimali za Chuma, Makaa ya Mawe;

- Kujenga viwanda vinavyotumia rasilimali za nchi hususan Magadi Soda, gesi-asili, Kemikali, saruji & vifaa vingine vya ujenzi, n.k;

2.3.2 Hatua Wezeshi kwa Ujenzi wa Uchumi wa Viwanda

(a) Kuendeleza Utulivu wa Uchumi Jumla

- Ukuaji wa Pato la Taifa wa wastani wa 8%
- Mfumuko wa Bei wa wastani wa 5%
- Utulivu wa kiwango cha kubadilisha fedha za kigeni
- Kuvutia Uwekezaji na Mitaji kutoka nje
- Kujitosheleza kwa Chakula na kuuza nje ziada
- Kuzalisha nishati ya kutosha
- Kuongeza mauzo nje ya bidhaa za viwandani

(b) Mapinduzi ya Kilimo

- Ukuaji wa Sekta ya Kilimo ufikie wastani wa 6% au zaidi kwa mwaka
- Kuongeza thamani, ubora na na viwango vya mazao ya kilimo
- Kuimarisha masoko ya mazao na barabara za vijijini
- Kuongeza uzalishaji na tija hasa kwa mazao yenye thamani kubwa (mbogamboga, viungo, matunda, maua, asali, mwani nk) & Kuongeza eneo la umwagiliaji
- Kuongeza mikopo kwa wakulima
- Kuhamasisha Ubia kati ya wakulima wadogo na wakubwa na wanaochakata mazao

(c) Hatua Nyingine

- Kuweka msukumo zaidi katika matumizi ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu kuongeza tija; Kutilia mkazo utoaji wa Elimu ya sayansi, teknolojia, ufundi, na kuimarisha ujuzi na ubunifu (Vyuo vya Ufundi Stadi, Polytechnics, Industrial Incubators, mafunzo ya ubunifu n.k hususan kwa vijana ambao ni wepesi kujifunza kutumia teknolojia mpya;

- Kuboresha miundombinu ya nishati, uchukuzi na huduma (logistics), kupiga vita rushwa na urasimu;

- Kuendelea kujenga uwezo wa kuzalisha umeme nchini (6,700 MW – 12,300MW ifikapo 2025)
- Kupunguza upotevu wa umeme hadi kufikia 15% katika usafirishaji na usambazaji wa umeme

Hatua Nyingine

- Kuimarisha usafiri wa abiria na uchukuzi wa mizigo kwa njia ya Barabara, Reli, Maji, Anga na Bomba
- Kutumia Ubia kati ya Sekta ya Umma na Binafsi
- Kuongeza kasi ya kupanga matumizi ya Ardhi na kuipima
- Kujenga nyumba za kisasa za gharama nafuu kwa wakazi – mijini & vijijini
- Kuimarisha upatikanaji wa huduma za Afya hasa vijijini na mafunzo ya wahudumu wa Afya
- Kuimarisha ushirikiano kati ya vyuo vya Elimu ya Juu na Viwanda
- Kujenga uwezo na ujuzi zaidi katika maeneo maalum hususan uendelezaji wa Gesi na Mafuta, Kioo na Chuma

3. Nafasi ya Mabalozi Katika Utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025

3.1 Diplomasia ya Kiuchumi

Moja ya kazi za msingi za Mabalozi ni kuongoza utekelezaji wa diplomasia ya kiuchumi kwa ufanisi, yaani kukuza maslahi ya kiuchumi na kibiashara ya Tanzania katika nchi husika ya kigeni. Kazi mahsusi ni:

- Kukuza biashara kati ya Tanzania na nchi husika ili kuongeza mauzo ya Tanzania nje;

- Kuhamasisha uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje kuja Tanzania (*FDI*) katika maeneo ya kipaumbele;

- Kuvutia shughuli zote zinazoiwezesha Tanzania kupata teknolojia bora zaidi;

- Kuhamasisha ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi kuwekeza hapa nchini;

- Kuitangaza Tanzania ili kukuza sekta ya utalii hapa nchini (kuvutia wawekezaji katika miundombinu ya utalii na watalii zaidi kutembelea Tanzania);

- Kuhimiza ushiriki wa sekta binafsi ya Tanzania katika maonyesho ya kibiashara nje ya nchi na kushawishi sekta binafsi ya nje kushiriki maonyesho ya kibiashara hapa nchini;

–Kuitambua Diaspora ya Tanzania na kuwashawishi kuchangia maendeleo ya Tanzania kupitia upelekaji wa fedha (*remittances*), utaalam/ujuzi, uwekezaji katika mali zisizohamishika, biashara, na kuitangaza Tanzania.

–Kutafuta fursa za mafunzo kwa Watanzania hususan katika maeneo maalum ya kimkakati (specialized skills & national strategic areas)

–Kushiriki kikamilifu katika majadiliano kuhusu mikataba ya kimataifa ya kibiashara katika taasisi mbalimbali kama vile WTO, Utangamano Afrika Mashariki, SADC, Maeneo huru ya kikanda (free trade agreements); na

–Kuendesha ujasusi wa kiuchumi (industrial & economic espionage) kwa maslahi ya Taifa.

3.2 Mwongozo wa Jumla :

3.2.1 Kila Balozi aijue vizuri nchi yake!

– Dira na vipaumbele vya Taifa;

– Taarifa muhimu (*facts /figures*) za Tanzania na nchi jirani/ kanda;

– Fursa zilizopo (*what can Tanzania offer*?);

–Kufuatilia mabadiliko Tanzania (*recent socio-economic devts*);

-Kufanya mawasiliano ya mara kwa mara na taasisi muhimu za kusimamia uchumi wa Taifa;

3.2.2 Kila Balozi afanye bidii kuifahamu nchi husika anakoiwakilisha Tanzania!

-Ajitume kukusanya & kuchambua taarifa muhimu (*Facts/ figures*, mikataba ya kibiashara na makubaliano baina ya nchi); Vipaumbele (*core economic interests – current & future*); mwenendo wa biashara na uchumi; na kuwatambua wahusika wakuu (*key players*) katika uchumi & biashara;

-Kutoa taarifa muhimu za uchumi & biashara za nchi husika kwa sekta binafsi ya Tanzania (fursa za masoko, masharti ya ubora wa bidhaa, mfumo wa kodi, fursa za ubia, mitaji n.k);

-Kujiwekea utaratibu wa kufanya mazungumzo (*networking*) na wasimamizi wakuu wa biashara na uchumi katika nchi husika na makampuni yanayoonesha nia ya kuja kuwekeza Tanzania hususan katika maeneo ya kipaumbele n.k.

-Fuateni mfano wa kuigwa wa Mhe. Rais Dr. Jakaya Mrisho Kikwete katika kukuza Diplomasia ya uchumi!

4. Hitimisho

- Tanzania yenye uchumi wa viwanda (*semi-industrialized country*) na kipato cha $3,000 ifikapo 2025 inawezekana!

- Kinachohitajika: Kutumia vizuri fursa za Tanzania (rasilimali, gesi asili, fursa zinazoambatana na ukuaji wa miji, jiografia, masoko ya kikanda & kimataifa, na nguvukazi ya Taifa mbayo kwa sehemu kubwa ni vijana.

- Jambo muhimu ni kufanya kazi tofauti na mazoea! hususan kuelekeza jitihada za diplomasia ya kiuchumi kwenye vipaumbele vichache na kuwa na malengo yanayopimika lakini pia pawepo *consequences* kwa kufanya vizuri au vibaya!;

- Diplomasia ya kiuchumi ina mchango mkubwa katika utekelezaji wa malengo ya Dira 2025. Lakini ni muhimu kuelekeza nguvu ya diplomasia ya kiuchumi kwenye *niche industries & services*, na kuendeleza rasilimali watu, kutegemea na fursa zilizopo katika nchi ambazo mnatuwakilisha. Msijitanue kushughulikia kila kitu cha kiuchumi!

-ORTM inatarajia kazi ya ziada hasa kutoka kwa Mabalozi wanaoliwakilisha Taifa katika nchi ambazo Tanzania inafanya nazo biashara kwa kiasi kikubwa hivi sasa (>40%) na kuna fursa kubwa zaidi za kuendeleza sekta ya viwanda hapa nchini au kuna soko kubwa la baadaye -- China, India, Japan, Ujerumani, UAE, Kenya na Afrika Kusini. Nchi nyingine za kutilia mkazo katika diplomasia ya kiuchumi ni USA, UK, Brazil, Malaysia, Vietnam, Korea Kusini na DRC.

ASANTENI KWA KUNISIKILIZA

Philip Mpango (Ph.D.)
Katibu Mtendaji – Ofisi ya Rais Tume ya Mipango
25 Mei, 2015